# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 994

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Somo la Kiswahili Elimu ya Msingi Darasa la III - VI

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-782-1

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Muhtasari wa Somo la Kiswahili Elimu ya Msingi Darasa la III - VI Tanzania Bara.

**Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa**
Kamishna wa Elimu

# MUHTASARI WA SOMO LA KISWAHILI

# ELIMU YA MSINGI DARASA LA III–VI

# 2023

MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 1 12/07/2023 20:42

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2023
Toleo la Kwanza, 2023

ISBN: 978-9987-09-782-1

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 735 041 168 / +255 735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). Muhtasari wa Somo la Kiswahili Elimu ya Msingi Darasa la III–VI. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa muhtasari huu au sehemu yake kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 2 12/07/2023 20:42

# Yaliyomo

Orodha ya Majedwali ..... iv
Vifupisho ..... v
Shukurani ..... vi
1.0 Utangulizi ..... 1
2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania ..... 1
3.0 Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la III–VI ..... 2
4.0 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Msingi Darasa la III–VI ..... 3
5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi ..... 3
6.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji ..... 4
6.1 Mwalimu ..... 5
6.2 Mwanafunzi ..... 6
6.3 Mzazi/ Mlezi ..... 6
7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji Zinazopendekezwa ..... 7
8.0 Zana/Vifaa vya Ufundishaji na Ujifunzaji Vinavyopendekezwa ..... 7
9.0 Upimaji ..... 7
10.0 Idadi ya Vipindi ..... 8
11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji ..... 8
Bibliografia ..... 70



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 3 12/07/2023 20:42

## Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi ........................................ 4

Jedwali Na. 2: Maudhui ya Darasa la III ........................................ 9

Jedwali Na. 3: Maudhui ya Darasa la IV ........................................ 26

Jedwali Na. 4: Maudhui ya Darasa la V ........................................ 42

Jedwali Na. 5: Maudhui ya Darasa la VI ........................................ 58

## Vifupisho

| | |
|---|---|
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 5 12/07/2023 20:42

## Shukurani

Maandalizi ya Muhtasari wa Somo la Kiswahili Elimu ya Msingi Darasa la III–VI yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za serikali na zisizo za serikali. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha uandaaji wa muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu, pamoja na wakuza mitaala wa TET. Vilevile, TET inaishukuru kwa dhati Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwaandaa wahitimu wenye maarifa, ujuzi na mwelekeo utakaowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndilo lengo kuu la uboreshaji wa Mitaala ya Mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.

Dkt. Aneth A. Komba

Mkurugenzi Mkuu

**Taasisi ya Elimu Tanzania**



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 6 12/07/2023 20:42

## 1.0 Utangulizi

Somo la Kiswahili ni somo la lazima katika ngazi ya Elimu ya Msingi kuanzia Darasa la III–VI ambapo ni mwendelezo wa hatua ya kwanza ya elimu ya msingi Darasa la I na la II. Lengo la kufundisha somo hili ni kukuza stadi za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika kwa Kiswahili. Mwanafunzi ataweza kutamka sauti mbalimbali katika silabi, maneno, sentensi na habari. Vilevile, mwanafunzi ataweza kujenga hoja kwa kuzungumza na kwa kuandika pamoja na kujibu hoja katika miktadha mbalimbali.

Muhtasari huu umeandaliwa kwa lengo la kumwongoza mwalimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili, Darasa la III–VI Tanzania Bara. Muhtasari huu umetafsiri Mtaala wa Elimu ya Msingi wa Mwaka 2023. Aidha, muhtasari utamwezesha mwalimu kupanga shughuli za ufundishaji na ujifunzaji kwa kumjengea mwanafunzi stadi za udadisi, ubunifu, ushirikiano, mawasiliano na utatuzi wa changamoto katika mazingira yake.

## 2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya elimu nchini Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;

(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Kitanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;

(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;

(d) Kuelewa na kulinda tunu za taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya taifa;

(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;

(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 1 12/07/2023 20:42

(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na

(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

## 3.0 Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa la III–VI

Malengo ya Elimu ya Msingi Darasa III–VI ni kumwezesha mwanafunzi:

(a) Kukuza stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu na kuwasiliana kwa lugha fasaha, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na lugha mguso;

(b) Kuifahamu, kuitumia na kuithamini lugha ya Kiswahili, Kiingereza na angalau lugha nyingine moja ya kigeni;

(c) Kuthamini na kudumisha utamaduni wa Mtanzania, umoja wa kitaifa na kutambua tamaduni nyingine;

(d) Kukuza maarifa, uwezo wa kudadisi, kufikiri kiyakinifu, kubuni na kutatua matatizo;

(e) Kukuza maadili, uadilifu na kuheshimu tofauti za imani;

(f) Kubaini na kukuza vipaji, vipawa, stadi za kazi, michezo na sanaa;

(g) Kukuza tabia ya kuthamini na kupenda kufanya kazi;

(h) Kutambua na kutumia sayansi na teknolojia katika kujifunza na maisha ya kila siku;

(i) Kukuza maarifa, ujuzi na mwelekeo wa kutunza mazingira, kuheshimu usawa wa kijinsia na masuala mengine mtambuka; na

(j) Kukuza uwezo wa kuchangamana katika mazingira jumuishi.



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 2 12/07/2023 20:42

## 4.0 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Msingi Darasa la III–VI

Umahiri wa jumla wa Elimu ya Msingi Darasa la III–VI ni:

(a) Kutumia stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu na kuwasiliana kwa lugha fasaha, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) na lugha mguso;

(b) Kutumia na kuithamini lugha ya Kiswahili, Kiingereza na angalau lugha nyingine moja ya kigeni;

(c) Kuonesha, kuthamini na kuheshimu utamaduni wa Mtanzania, umoja wa kitaifa na kutambua tamaduni nyingine;

(d) Kudadisi, kufikiri kiyakinifu, kubuni na kutatua matatizo;

(e) Kuonesha uadilifu na kuheshimu tofauti za imani;

(f) Kutumia vipaji, vipawa, stadi za kazi, michezo na sanaa katika miktadha mbalimbali;

(g) Kuthamini na kupenda kufanya kazi;

(h) Kutumia sayansi na teknolojia katika kujifunza na maisha ya kila siku;

(i) Kutunza mazingira, kuheshimu usawa wa kijinsia na masuala mengine mtambuka; na

(j) Kuchangamana katika mazingira jumuishi.

## 5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi

Umahiri mkuu na umahiri mahususi unaotarajiwa kujengwa kwa Darasa la III–VI umebainishwa katika Jedwali Na. 1.



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 3 12/07/2023 20:42

**Jedwali Na. 1:** *Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Darasa la III–VI*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 1.1 Kutambua matamshi ya sauti mbalimbali katika silabi, maneno, sentensi na habari<br>1.2 Kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali<br>1.3 Kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali |
| 2.0 Kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma | 2.1 Kuonesha stadi za kusikiliza na kuelewa<br>2.2 Kusoma matini kwa ufasaha na ufahamu |
| 3.0 Kuwasilisha hoja kwa mazungumzo na kwa maandishi kulingana na muktadha | 3.1 Kuwasilisha hoja kwa njia ya mazungumzo katika miktadha mbalimbali<br>3.2 Kuandika matini mbalimbali<br>3.3 Kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali<br>3.4 Kuonesha stadi za awali za ubunifu wa kazi mbalimbali za Kiswahili |

## 6.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji unategemea ushirikiano madhubuti baina ya mwalimu, mwanafunzi na mzazi/mlezi katika kutekeleza majukumu mbalimbali. Majukumu hayo ni kama yafuatayo:



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 4 12/07/2023 20:42

## 6.1 Mwalimu

Mwalimu anatarajiwa:

(a) Kumwezesha mwanafunzi kujifunza na kupata umahiri uliokusudiwa katika somo la Kiswahili;

(b) Kutumia mbinu za kufundishia na kujifunzia kwa kuzingatia umri, mahitaji anuai na uwezo wa mwanafunzi ili kumwezesha:

(i) Kujenga umahiri unaohitajika katika Karne ya 21; na

(ii) Kushiriki kikamilifu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

(c) Kutumia mbinu shirikishi zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji zikiwemo zile zinazomwezesha mwanafunzi kufikiri, kutafakari na kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali. Mbinu za kufundishia na kujifunzia zinazopendekezwa ni pamoja na kazi za vitendo, utafiti, majaribio ya kisayansi, majadiliano na kazimradi zinazolenga kutatua matatizo halisi katika mazingira ya mwanafunzi. Aidha, mwalimu anahimizwa kutumia njia nyingine kama hizo kulingana na muktadha ili kufanikisha ujenzi wa umahiri uliokusudiwa;

(d) Kuandaa darasa salama lenye mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia;

(e) Kutengeneza au kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia;

(f) Kufanya upimaji endelevu mara kwa mara kwa kutumia zana na mbinu za upimaji na tathmini zinazopima nadharia na vitendo zikiwemo bunguabongo, orodhahakiki, majaribio, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi na kazi za vikundi), kazimradi na mkoba wa kazi. Zana na mbinu nyingine ni majaribio kwa vitendo, uwasilishaji, mitihani ya muhula na mtihani wa mwisho;

(g) Kuhakikisha kuwa ufundishaji na ujifunzaji unafanyika kwa haki na usawa kwa kila mwanafunzi bila kujali tofauti zao;



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 5 12/07/2023 20:42

(h) Kumlinda mwanafunzi awapo shuleni;

(i) Kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi ya kila siku;

(j) Kubaini mahitaji ya mwanafunzi na kutoa afua stahiki;

(k) Kushirikisha wazazi/walezi na jamii katika hatua mbalimbali za ujifunzaji wa mwanafunzi; na

(l) Kuchopeka masuala mtambuka na TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

**6.2 Mwanafunzi**

Mwanafunzi anatarajiwa:

(a) Kuwa mtendaji mkuu katika mchakato wote wa ujifunzaji;

(b) Kushiriki katika shughuli mbalimbali za ujifunzaji ndani na nje ya darasa ili kupata umahiri unaokusudiwa; na

(c) Kushiriki katika kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo vitabu vya kiada, ziada na machapisho mengine kutoka katika maktaba mtandao.

**6.3 Mzazi/Mlezi**

Mzazi/ Mlezi anatarajiwa:

(a) Kusimamia na kufuatilia maendeleo ya mtoto katika ujifunzaji;

(b) Kumsimamia mtoto kutekeleza kazi zake za kitaaluma pale inapowezekana;

(c) Kuhakikisha kuwa mazingira ya nyumbani ni rafiki na salama yanayowezesha ujifunzaji;

(d) Kufuatilia mwenendo wa tabia ya mtoto;

(e) Kumpatia mtoto vifaa vyote vinavyohitajika katika ujifunzaji;

(f) Kuhakikisha mtoto anapata mahitaji muhimu; na

(g) Kumfundisha mtoto umuhimu na thamani ya elimu na kazi pamoja na kumuhimiza kujifunza kwa bidii.

## 7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji ni msingi katika kujenga umahiri kwa mwanafunzi. Muhtasari huu unapendekeza mbinu za ufundishaji na ujifunzaji kwa kila shughuli. Miongoni mwa mbinu hizo ni ziara za kimasomo, kazimradi na kazi za vitendo. Hata hivyo, mwalimu anashauriwa kutumia mbinu nyingine kama hizo kulingana na muktadha wa ufundishaji na ujifunzaji.

## 8.0 Zana/Vifaa vya Ufundishaji na Ujifunzaji

Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unahitaji zana/vifaa mbalimbali ili kujenga umahiri uliokusudiwa. Hivyo, mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kushirikiana katika kuandaa au kufaragua zana/vifaa mbadala vinavyopatikana katika mazingira ya shuleni na nyumbani pindi vinapohitajika. Mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kutafuta taarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali ili kuleta ufanisi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Mwalimu anapaswa kuhakikisha kuwa mwanafunzi anapata nafasi ya kuona, kunusa, kuonja, kusikia na kushika zana bila kuhatarisha afya na hali ya mwanafunzi. Orodha ya vifaa vilivyoidhinishwa kutumika kwa ajili ya rejea vitatolewa na TET.

## 9.0 Upimaji

Upimaji ni suala muhimu katika mchakato wa ujifunzaji na ufundishaji ili kuwezesha ujenzi wa umahiri unaokusudiwa. Upimaji wa Somo la Kiswahili utajumuisha upimaji endelevu na upimaji tamati. Upimaji endelevu utazingatia vigezo vya upimaji vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji na utamwezesha mwalimu kubaini uwezo na uhitaji wa mwanafunzi katika ujifunzaji. Vilevile, utalenga kupima mabadiliko katika maarifa, stadi na mwelekeo wa kutenda, kuthamini, kusimulia na kutumia stadi anazojifunza katika mazingira yanayomzunguka. Aidha, mwalimu atatumia taarifa za upimaji kuboresha ufundishaji na kuwezesha wanafunzi kufikia lengo la ujifunzaji. Zana za upimaji zinazoweza kutumika wakati wa ufundishaji na ujifunzaji ni bunguabongo, orodhahakiki, mazoezi ya darasani, majaribio, majaribio kwa vitendo, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi na kazi za vikundi), kazimradi, mkoba wa kazi na zana nyingine kama hizo.



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 7 12/07/2023 20:42

Upimaji tamati utahusisha mitihani ya wiki, mwezi, muhula na mtihani wa mwisho wa mwaka ambayo itatumika kupima maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi. Taarifa za upimaji huu pamoja na kutumika kutathimini maendeleo ya mwanafunzi, zitatumika kutoa mrejesho wa kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, kutakuwa na Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Sita ambao utachangia alama 7.5% katika mtihani wa Kidato cha Nne.

## 10.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa Somo la Kiswahili Elimu ya Msingi Darasa la III–VI unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwanafunzi. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi, ambapo kila kipindi ni dakika 40. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni vitano (5) kwa wiki kwa Darasa la III–VI.

## 11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Maudhui ya ufundishaji na ujifunzaji yamepangiliwa katika jedwali lenye vipengele saba ambavyo ni; umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa, vigezo vya upimaji, zana/vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa pamoja na idadi ya vipindi. Maudhui hayo yameoneshwa katika Jedwali Na. 2–5.



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 8 12/07/2023 20:42

## Darasa la III

**Jedwali Na. 2:** *Maudhui ya Darasa la III*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 1.1 Kutambua matamshi ya sauti mbalimbali katika silabi, maneno, sentensi na habari | (a) Kutamka sauti za herufi mwambatano *ngw*, *ndw, njw*, *mbw* na *nzw* | **Oneshombinu:** Waongoze wanafunzi kutamka herufi za sauti mwambatano *ngw*, *ndw, njw*, *mbw* na *nzw* kwa kufuatisha unavyotamka au waoneshe wanafunzi video ya utamkaji wa sauti za herufi mwambatano tajwa kisha waongoze kutamka sauti za herufi hizo<br>**Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kujibu maswali ambayo yana majibu yenye sauti za herufi mwambatano *ngw*, *ndw, njw*, *mbw* na *nzw* | Sauti za herufi mwambatano *ngw*, *ndw, njw*, *mbw* na *nzw* zimetamkwa kwa usahihi | Kadi za herufi mwambatano, matini zenye vifungu vya habari vyenye sauti za herufi mwambatano *ngw*, *ndw, njw*, *mbw* na *nzw*, manila, kalamu rashasha, chatipindu, video na tableti | 21 |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 9 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini zenye sauti za herufi mwambatano *ngw*, *ndw, njw*, *mbw* na *nzw,* kisha wazibainishe herufi hizo<br><br>**Mchezo:** Tumia kadi za maneno/vyumba vya kuchora chini kuwaongoza wanafunzi kutamka sauti za herufi mwambatano *ngw*, *ndw, njw*, *mbw* na *nzw.* Kwa kila chumba, andika herufi mwambatano moja | | | |
| | | (b) Kutamka sauti mwambatano katika silabi, maneno, sentensi na habari | **Igizodhima:** Waongoze wanafunzi kuigiza utendaji wa shughuli mbalimbali, ambapo ndani yake watatumia sauti za herufi mwambatano | Sauti za herufi mwambatano katika silabi, maneno, sentensi na habari zimetamkwa kwa usahihi | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Kitanza ndimi:** Waongoze wanafunzi kusoma sentensi zenye maneno yenye sauti za herufi mwambatano zinazofuatana | | | |
| | 1.2 Kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali | (a) Kutumia msamiati unaohusiana na maisha ya kila siku katika kuanzisha na kuendeleza mazungumzo kwa kujiamini katika miktadha mbalimbali | **Igizodhima:** Waongoze wanafunzi kuigiza shughuli za kila siku katika miktadha tofautitofauti kwa kutumia msamiati mwafaka na kwa kujiamini<br><br>**Mchezo wa maneno:** Waongoze wanafunzi kuunda maneno kwa kuanza na kila herufi ya neno linalohusiana na maisha ya kila siku | Msamiati unaohusiana na maisha ya kila siku umetumika katika kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali kwa kujiamini | Picha, michoro, vitu halisi, sidii, kinasasauti na kompyuta | 22 |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 11 12/07/2023 20:42

| **Umahiri mkuu** | **Umahiri mahususi** | **Shughuli za ujifunzaji** | **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | **Vigezo vya upimaji** | **Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa** | **Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kubaini maneno yenye maana sawa na kinyume katika mazungumzo | **Hadithi:** Waongoze wanafunzi kubainisha maneno yenye maana sawa na vinyume kutoka kwenye mazungumzo<br><br>**Ziara:** Waongoze wanafunzi kufanya ziara ili kubaini majina ya vitu vyenye maana sawa na vinyume vya maneno, kisha kuwasilisha | Maneno yenye maana sawa na kinyume yamebainishwa kwa usahihi katika mazungumzo | | |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 12 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kuelezea vitu vilivyomo kwenye mazingira katika umoja na wingi | **Uchunguzi:** Waongoze wanafunzi kuchunguza vitu vilivyomo kwenye mazingira yao, kisha wabainishe umoja na wingi wa vitu hivyo<br>**Oneshombinu**: Waongoze wanafunzi kubainisha umoja na wingi wa vitu mbalimbali utakavyowaonesha | Vitu vilivyomo kwenye mazingira vimeelezewa kwa usahihi katika umoja na wingi | | |
| | | (d) Kuuliza na kujibu maswali | **Majadiliano**: Waongoze wanafunzi kujadiliana mada yoyote fulani, kisha waulizane maswali<br>**Mkufu:** Waongoze wanafunzi kuulizana maswali na kujibu kwa mfuatano wa kimkufu | Maswali yameulizwa na kujibiwa kwa ufasaha | | |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 13 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (e) Kubadili kiimbo kulingana na hisia au muktadha wa mazungumzo | **Masimulizi:** Waongoze wanafunzi kusimulia matukio mbalimbali ili kubadili kiimbo na kuonesha hisia tofautitofauti | Kiimbo kimebadilishwa kulingana na hisia au muktadha wa mazungumzo kwa usahihi | | |
| | | (f) Kuanzisha na kumalizia vitendawili, methali na nahau katika mazungumzo | **Uchunguzi:** Waongoze wanafunzi kwa kutumia picha/vitu halisi kutega na kutegua vitendawili, kuanzisha na kumalizia methali na kueleza maana ya nahau na methali | Vitendawili, methali na nahau vimeanzishwa na kumaliziwa kwa usahihi katika mazungumzo | | |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 14 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Mchezo:** Waongoze wanafunzi katika timu mbili kutega na kutegua vitendawili, kuanzisha na kumalizia methali na kueleza maana ya nahau | | | |
| | 1.3 Kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali | (a) Kuandika kifungu cha habari kwa kutumia alama za uakifishaji: nukta (.), mshangao (!), kiulizo (?) na mkato (,) | **Imla:** Wasomee wanafunzi kifungu cha habari ulichokiandaa na wakiandike kwa kutumia alama za uakifishaji: nukta (.), mshangao (!), kiulizo (?) na mkato (,) | Kifungu cha habari kimeandikwa kwa kutumia alama za uakifishaji kwa usahihi: nukta (.), mshangao (!), kiulizo (?) na mkato (,) | Kompyuta, tableti, kadi za alama za uakifishaji, picha, kifungu cha habari na vitu halisi | 22 |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 15 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kuandika kifungu cha habari kwa kutumia viunganishi vya ushikamani | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kusoma matini, kisha wabainishe na kujadili maneno yanayofanya kazi ya kuonesha uhusiano au muungano baina ya sentensi na sentensi au vifungu vya maneno (kifungu cha maneno na kifungu cha maneno) | Kifungu cha habari kimeandikwa kwa kutumia viunganishi vya ushikamani | | |
| | | (c) Kutumia alama za uakifishaji kwa usahihi wakati wa kuandika imla | **Majadiliano**: Waongoze wanafunzi kujadiliana umuhimu na matumizi sahihi ya alama za uakifishaji, kisha waandike imla kwa kuzingatia alama hizo | Alama za uakifishaji zimetumika kwa usahihi wakati wa kuandika imla | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Masimulizi:** Waongoze wanafunzi kusikiliza masimulizi yaliyorekodiwa, kisha waandike walichokisikia kwa kuzingatia alama za uakifishaji | | | |
| | | (d) Kutumia vihusishi (*nyuma ya, mbele ya, juu ya, kando ya, chini ya, katikati ya* na *pembeni ya*) katika uandishi | **Oneshombinu**: Waoneshe wanafunzi vitu halisi au picha ulizoziandaa, kisha waongoze kubainisha mahali vitu vilipo kwa kuzingatia vihusishi vilivyobainishwa | Vihusishi (*nyuma ya, mbele ya, juu ya, kando ya, chini ya, katikati ya* na *pembeni ya*) vimetumika katika uandishi kwa usahihi | | |

| **Umahiri mkuu** | **Umahiri mahususi** | **Shughuli za ujifunzaji** | **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | **Vigezo vya upimaji** | **Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa** | **Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2.0 Kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma | 2.1 Kuonesha stadi za kusikiliza na kuelewa | (a) Kusikiliza mazungumzo kwa kuzingatia mambo ya msingi katika miktadha mbalimbali | **Masimulizi**: Waongoze wanafunzi kusimuliana hadithi au habari, kisha wajibu maswali kwa kuzingatia mambo ya msingi katika miktadha mbalimbali | Mazungumzo kwa kuzingatia mambo ya msingi katika miktadha mbalimbali yamesikilizwa | Sidii, kompyuta, redio, tableti na kamusi | 22 |
| | | (b) Kutumia maneno aliyoyasikia katika miktadha mingine ya mazungumzo | **Oneshombinu**: Waoneshe wanafunzi picha au vitu halisi, kisha waongoze kutumia maneno yanayoendana na vitu hivyo kulingana na muktadha | Maneno aliyoyasikia katika miktadha mingine ya mazungumzo yametumika kwa usahihi | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kutumia kamusi kupata maana ya msamiati mpya uliojitokeza katika matini fupi sahili | **Hadithi:** Andaa hadithi inayoonesha kazi ya kamusi<br>**Kazimradi:** Wape wanafunzi maneno kadhaa kutokana na matini fupi sahili, kisha watafute fasili kwenye kamusi | Kamusi imetumika kupata maana ya msamiati mpya uliojitokeza katika matini fupi sahili | | |
| | | (d) Kujibu kwa usahihi maswali yanayotokana na matini | **Midia:** Waongoze wanafunzi kusikiliza habari iliyopo katika matini, kisha waulize maswali kuhusiana na matini hiyo<br>**Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kujadiliana kwa kutumia matini umuhimu wa elimu, kisha waulize maswali | Maswali yanayotokana na matini yamejibiwa kwa usahihi | | |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 19 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2.2 Kusoma matini kwa ufasaha na ufahamu | (a) Kusoma matini fupi na sahili kwa kasi mwafaka na matamshi sahihi | **Oneshombinu:** Soma matini fupi na rahisi kwa kasi mwafaka kulingana na umri wa wanafunzi wako, matamshi sahihi, kiimbo na alama za uakifishaji kama mfano, kisha waongoze wao kusoma | Matini fupi na sahili zimesomwa kwa kasi mwafaka na matamshi sahihi | Matini fupi sahili, saa, kinasasauti, simujanja, redio, kompyuta, tableti na kinyonyi | 22 |
| | | (b) Kusoma sentensi kwa kuzingatia kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti | **Uchunguzi:** Waongoze wanafunzi kubaini sentensi zenye mipando tofauti ya sauti kwa kutumia vifaa vya TEHAMA, kisha waongoze kurudia kutamka sentensi hizo ili kuonesha viimbo tofauti | Sentensi zimesomwa kwa kuzingatia kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti kwa ufasaha | | |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 20 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Maswali na Majibu:** Waongoze wanafunzi kutunga sentensi, kisha wazisome kwa sauti kwa kuzingatia kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti | | | |
| | | (c) Kueleza ujumbe mkuu uliomo katika matini fupi aliyoisoma | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi, kisha waulize maswali kuhusu ujumbe mkuu kutokana na matini | Ujumbe mkuu uliomo katika matini fupi iliyosomwa umeelezwa kwa ufasaha | | |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 21 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3.0 Kuwasilisha hoja kwa mazungumzo na kwa maandishi kulingana na muktadha | 3.1 Kuandika matini mbalimbali | (a) Kuandika sentensi mbalimbali kwa usahihi | **Mchezo:** Andaa sentensi, kisha kata sentensi hizo katika maneno na kadi hizo za maneno zichanganye. Waongoze wanafunzi kuunda sentensi na kuziandika kwa kutumia maneno hayo yaliyoandikwa kwenye kadi | Sentensi mbalimbali zimeandikwa kwa usahihi | Kadi za sentensi na picha za matukio | 22 |
| | | (b) Kupanga katika mtiririko sahihi sentensi zilizochanganywa | **Maswali na majibu:** Andaa sentensi zenye mpangilio wa maneno usio sahihi, kisha waongoze wanafunzi kuandika sentensi hizo kwa usahihi | Sentensi zilizochanganywa zimepangwa katika mtiririko sahihi | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Ziara:** Waongoze wanafunzi kutembelea shule ya jirani, kisha wasimulie ziara yao hatua kwa hatua. Ziandike hatua hizo kwa kutumia sentensi kamili, kisha zichanganye sentensi hizo na kuwataka wanafunzi kuzipanga kwa mfuatano wa kimantiki | | | |
| | | (c) Kuandika matini fupi kwa kuzingatia mpangilio sahihi wa maneno na alama za uakifishaji | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kujadili kuhusu mpangilio sahihi wa maneno na umuhimu wa alama za uakifishaji katika uandishi wa matini fupi, kisha waandike matini fupi kwa kuzingatia mambo hayo | Matini fupi imeandikwa kwa usahihi kwa kuzingatia mpangilio sahihi wa maneno na alama za uakifishaji | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 3.2 Kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali | (a) Kubainisha msamiati uliojitokeza katika matini fupi sahili | **Kazimradi:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi sahili na kusikiliza habari kwenye televisheni, redio au simu, kisha wabainishe msamiati uliomo pamoja na fasili zake<br><br>**Hadithi:** Waongoze wanafunzi kusoma au kusikiliza hadithi, kisha wataje maneno mapya na watafute maana zake katika kamusi | Msamiati uliojitokeza katika matini fupi sahili umebainishwa | Matini fupi sahili, redio, kamusi na televisheni | 22 |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 24 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kuchambua mawazo makuu yanayojitokeza katika matini fupi sahili | **Changanyakete:** Gawa matini tofauti katika vikundi, waongoze wanafunzi kusoma na kuandika ujumbe wa matini hizo, kisha kila kikundi kihakikishe kinasoma kazi zote na kueleza masuala muhimu yaliyomo kwenye matini husika | Mawazo makuu yaliyojitokeza katika matini fupi sahili yamechambuliwa kwa ufanisi | | |
| | 3.3 Kuonesha stadi za awali za ubunifu wa kazi mbalimbali za Kiswahili | (a) Kusimulia hadithi fupi sahili | **Masimulizi:** Waongoze wanafunzi kusimuliana hadithi, kisha chagua wanafunzi wachache wasimulie hadithi zao mbele ya darasa | Hadithi fupi sahili zimesimuliwa kwa usahihi | Michoro, hadithi fupi sahili, vielelezo na picha | 22 |

## Darasa la 1V

**Jedwali Na. 3**: *Maudhui ya Darasa la IV*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 1.1 Kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali | (a) Kulinganisha vitu kwa kutumia maneno (*kuliko, zaidi ya, kama, mithili ya* na *mfano wa*) katika miktadha mbalimbali | **Oneshombinu:** Onesha vitu viwiliviwili, kisha waongoze wanafunzi kueleza dhana ya ulinganishi<br>**Maswali na majibu:** Andaa jedwali lenye maneno ya kulinganisha, kisha waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia jedwali | Vitu vimelinganishwa kwa kutumia maneno (*kuliko, zaidi ya, kama, mithili ya* na *mfano wa)* katika miktadha mbalimbali kwa ufasaha | Orodha ya nahau na methali, vitu halisi, michoro na picha | 38 |
| | | (b) Kusimulia matukio kwa kuzingatia njeo za | **Ramani ya dhana:** Waongoze wanafunzi kupitia mchoro kueleza aina za nyakati na hali | Matukio yamesimuliwa kwa usahihi katika nyakati na hali mbalimbali | | |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 26 12/07/2023 20:42

| **Umahiri mkuu** | **Umahiri mahususi** | **Shughuli za ujifunzaji** | **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | **Vigezo vya upimaji** | **Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa** | **Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | wakati: uliopo (-na-), uliopita (-li-), ujao (-ta-); na hali timilifu (-me-) na mazoea (hu-) | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kuzingatia viambishi vya nyakati na hali | | | |
| | | (c) Kujieleza kwa kujiamini | **Mdahalo:** Wape mada wanafunzi na wagawe katika vikundi viwili, kisha waongoze kufanya majibizano kwa kujiamini<br><br>**Igizo:** Waongoze wanafunzi kuigiza kwa kujiamini | Kujieleza kwa kujiamini kumefanyika kwa ufasaha | | |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 27 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) Kuunga mkono au kupinga wazo kwa hoja na mifano rahisi | **Ngonjera:** Wape wanafunzi mada na uhusika kisha ongoza majibizano yao na wafanye majumuisho ya hoja zilizoibuliwa | Wazo limeungwa mkono na kupingwa kwa hoja na mifano rahisi | | |
| | | (e) Kutumia nahau na methali katika mazungumzo | **Picha na maelezo:** Chora picha na uweke nahau na methali kwa kila picha halafu waongoze wanafunzi kutambua uhusiano wa nahau, methali na picha zake, kisha watumie nahau na methali hizo kwa kuzingatia maana zake | Nahau na methali zimetumiwa vizuri katika mazungumzo | | |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 28 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Hadithi:** Waongoze wanafunzi kutunga hadithi kwa kutumia nahau na methali | | | |
| | 1.2 Kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali | (a) Kutunga matini sahili kwa kutumia alama za uakifishaji: kistari kifupi (-), mkwaju (/), mabano ( ) na funga na fungua semi (“ ”) | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kutunga matini sahili kwa kutumia vielelezo vya alama za uakifishaji kwa usahihi | Matini sahili zimetungwa kwa kutumia alama za uakifishaji: kistari kifupi (-), mkwaju (/), mabano ( ) na funga na fungua semi (“ ”) kwa usahihi | Barua za kirafiki, bahasha, stempu, kompyuta, tableti na kadi za alama za uakifishaji | 30 |
| | | (b) Kutumia nyakati na hali kwa usahihi katika uandishi wa kifungu cha habari | **Kusoma matini:** Andaa matini zilizotumia nyakati na hali mbalimbali, kisha waongoze wanafunzi kubaini nyakati na hali hizo | Nyakati na hali vimetumika kwa usahihi katika uandishi wa kifungu cha habari | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | kwa kupigia mstari, halafu watunge sentensi kwa kutumia nyakati na hali hizo | | | |
| | | (c) Kuandika matini sahili kwa kuzingatia mtiririko sahihi wa mawazo | **Masimulizi:** Andaa picha zenye kujenga habari, zichanganye, kisha waongoze wanafunzi kuandika habari kwa kuzingatia mfuatano sahihi wa picha walizopewa | Matini sahili imeandikwa kwa kuzingatia mtiririko sahihi wa mawazo | | |
| | | (d) Kuandika barua ya kirafiki kwa kuzingatia muundo sahihi | **Majadiliano:** Gawa barua za kirafiki katika vikundi, kisha waongoze wanafunzi kujadili vipengele vyake | Barua ya kirafiki imeandikwa kwa kuzingatia muundo sahihi | | |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 30 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Majigambo:** Wape wanafunzi uhusika wa vipengele vya barua ya kirafiki, kisha waongoze kujigamba mbele ya darasa kulingana na sifa za vipengele hivyo | | | |
| 2.0 Kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma | 2.1 Kuonesha stadi za kusikiliza na kuelewa | (a) Kusikiliza hadithi | **Hadithi:** Waongoze wanafunzi kusikiliza hadithi kwenye redio/televisheni/kinasasauti, kisha waulize maswali kutokana na hadithi waliyoisikiliza<br>**Masimulizi:** Waongoze wanafunzi kusimulia hadithi waliyoisikiliza | Hadithi imesikilizwa kwa umakini | Hadithi, kinasasauti, sidii, kompyuta, tableti na redio | 30 |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 31 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kubaini hisia za msimuliaji kutokana na kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti | **Hadithi: S**imulia hadithi kwa kuuvaa uhusika wa kila mhusika kwa kuzingatia kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti, kisha waongoze wanafunzi kutaja sifa za kila mhusika kwa kuzingatia uhusika wake | Hisia za msimuliaji zimebainishwa kwa usahihi kutokana na kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti | | |
| | | (c) Kubaini ujumbe mkuu kutokana na hadithi aliyoisikiliza | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili ujumbe mkuu kutokana na hadithi waliyoisikiliza | Ujumbe mkuu katika hadithi iliyosikilizwa umebainishwa | | |

| **Umahiri mkuu** | **Umahiri mahususi** | **Shughuli za ujifunzaji** | **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | **Vigezo vya upimaji** | **Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa** | **Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2.2 Kusoma matini kwa ufasaha na ufahamu | (a) Kusoma matini fupi sahili kwa ufasaha | **Ziara:** Waelekeze wanafunzi kwenda maktaba kusoma matini fupi sahili, kisha warudi darasani na wasimuliane matini hizo<br>**Kusoma kwa sauti**: Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi sahili kwa sauti kwa kuzingatia kasi stahiki, matamshi sahihi na alama za uakifishaji | Matini fupi sahili imesomwa kwa ufasaha | Matini fupi sahili na kamusi | 22 |
| | | (b) Kujibu maswali kutokana na matini fupi aliyoisoma | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kujibu maswali yanayohusiana na matini walizozisoma | Maswali kutokana na matini fupi iliyosomwa yamejibiwa kwa usahihi | | |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 33 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Karatasi tembezi:** Gawa maswali tofautitofauti yanayohusu matini, kisha kila kikundi kiandike majibu kwenye karatasi na kigawe karatasi yenye majibu kwenye vikundi vingine kwa ajili ya kusoma majibu ya vikundi hivyo | | | |
| | | (c) Kutumia msamiati na semi mpya zilizomo kwenye matini fupi aliyoisoma | **Kusoma matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi na kubaini msamiati na semi mpya kwenye kazi bunifu | Msamiati na semi mpya zilizomo kwenye matini fupi aliyoisoma vimetumiwa kwa usahihi | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kutunga habari kwa kutumia msamiati na semi mpya kutoka kwenye matini fupi walizozisoma | | | |
| 3.0 Kuwasilisha hoja kwa mazungumzo na kwa maandishi kulingana na muktadha | 3.1 Kuwasilisha hoja kwa njia ya mazungumzo katika miktadha mbalimbali | (a) Kubaini msamiati au vifungu vya maneno vinavyotumika kujenga au kupinga hoja (mf. *hoja yako ni nzuri lakini ..., ingawa unasema hivi, kuna ...)* | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kusikiliza mada katika vyombo vya habari au vifaa vya TEHAMA, kisha wabaini msamiati au vifungu vya maneno vinavyotumika kujenga au kupinga hoja | Msamiati au vifungu vya maneno vinavyotumika kujenga au kupinga hoja vimebainishwa kwa usahihi | Kamusi na matini mbalimbali | 20 |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 35 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Mdahalo**: Waongoze wanafunzi kujenga au kupinga hoja kwa kutumia msamiati mwafaka na vifungu vya maneno vinavyotumika kujenga au kupinga hoja | | | |
| | | (b) Kutoa maoni au mawazo kwa kutumia msamiati na vifungu vya maneno vinavyotumika kujenga au kupinga hoja | **Mdahalo:** Waongoze wanafunzi kujenga hoja au kupinga hoja kwa kutumia msamiati mwafaka na vifungu vya maneno kwa usahihi<br>**Mchezo:** Waongoze wanafunzi kuigiza wapo kwenye kikao cha darasa kinachojadili namna ya kufanya usafi wa darasa kwa kutumia lugha mwafaka | Maoni au mawazo kwa kutumia msamiati na vifungu vya maneno vinavyotumika kujenga au kupinga hoja yametolewa kwa staha | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kujenga hoja kwa mfuatano na ushikamani wa kimantiki | **Mchezo:** Andika sentensi kadhaa zinazojenga wazo moja (kila sentensi iwe kwenye karatasi yake), wape wanafunzi sentensi mojamoja na hakikisha wamechanganyika, kisha wajipange kwa mfuatano kulingana na mantiki ya sentensi<br><br>**Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kuoanisha sentensi kwenye safu mbili | Hoja zimejengwa kwa mfuatano na ushikamani wa kimantiki | | |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 37 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 3.2 Kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali | (a) Kusoma matini fupi sahili | **Usomaji wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi sahili kwa sauti na kimya, kisha waulize maswali kuhusu matini waliyoisoma<br><br>**Ziara:** Waongoze wanafunzi kutembelea maktaba ya karibu ili kusoma matini mbalimbali kwa kuzingatia mwongozo uliowapa, kisha waandike waliyoyasoma na kuwasilisha darasani | Matini fupi sahili zimesomwa | Matini fupi sahili na kamusi | 22 |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 38 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kueleza maana ya semi mpya zilizojitokeza katika matini fupi sahili | **Usomaji wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini na kubaini msamiati na semi mpya kwenye matini<br>**Kazimradi:** Waongoze wanafunzi kwa kutumia kamusi kutafuta maana za msamiati na semi mpya zilizojitokeza kwenye matini<br>**Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kutunga sentensi kwa kutumia msamiati na semi mpya kutoka kwenye matini | Maana ya semi mpya zilizojitokeza katika matini zimeelezwa kwa usahihi | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kuwasilisha mawazo makuu yaliyomo katika matini fupi sahili | **Usomaji wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini fupi sahili, kisha wazifupishe kwa kuzingatia mawazo makuu yaliyomo katika matini hizo<br><br>**Mchezo:** Waongoze wanafunzi, katika safu mbili, kwa kushindana, kuwasilisha mawazo yaliyomo kwenye matini walizosoma, kisha toa alama kwa kila wazo. Safu yenye alama nyingi ndiyo itakayoshinda | Mawazo makuu yaliyomo katika matini fupi sahili yamewasilishwa kwa usahihi | | |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 40 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 3.3 Kuonesha stadi za awali za ubunifu wa kazi mbalimbali za Kiswahili | (a) Kutunga hadithi fupi sahili | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kusoma hadithi fupi sahili, wajadiliane mambo ya kuzingatia katika utunzi wa hadithi, kisha watunge hadithi fupi sahili<br><br>**Masimulizi:** Waongoze wanafunzi kusimulia maisha yao wawapo shuleni<br><br>**Igizo:** Waongoze wanafunzi kuigiza hadithi waliyoisimulia kuhusu maisha yao wawapo shuleni | Hadithi fupi sahili zimetungwa vizuri | Picha, vielelezo, michoro na hadithi fupi sahili | 15 |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 41 12/07/2023 20:42

## Darasa la V

**Jedwali Na. 4:** *Maudhui ya Darasa la V*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 1.1 Kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali | (a) Kutumia msamiati katika kusimulia matukio, habari na vitu mbalimbali kwa kujiamini | **Oneshombinu:** Waoneshe wanafunzi picha zilizo katika mfuatano kusimulia matukio, habari na masuala mbalimbali kwa kujiamini | Msamiati umetumika katika kusimulia matukio, habari na vitu mbalimbali kwa kujiamini | Kamusi, orodha ya methali na nahau | 21 |
| | | (b) Kubainisha nafsi (*umoja na wingi)* katika mazungumzo | **Picha na maelezo:** Onesha picha zinazobainisha nafsi (umoja na wingi) yaani | Nafsi tatu (*umoja* na *wingi*) katika mazungumzo zimebainishwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | watu wakiwa kwenye shughuli mbalimbali, kisha eleza nafsi tatu katika umoja na wingi wake<br><br>**Mchezo:** Ongoza mchezo wa kutunga sentensi kwa kuzingatia nafsi. Safu ya kwanza iwe nafsi ya kwanza umoja na wingi. Fanya hivyo kwa safu ya pili na ya tatu. Zingatia kuwa sentensi moja itabadilishwa katika nafsi zote | | | |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 43 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kutumia nahau na methali katika mazungumzo | **Masimulizi:** Waongoze wanafunzi kusimulia hadithi kwa kutumia nahau na methali kwa usahihi | Nahau na methali zimetumika kwa usahihi katika mazungumzo | | |
| | 1.2 Kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali | (a) Kuandika kifungu cha habari kwa kuzingatia alama za uakifishaji: nuktapacha (:), nuktamkato (;), ritifaa (‘) na nuktakatishi (…) | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kujadili matumizi ya alama za uakifishaji: nuktapacha (:), nuktamkato (;), ritifaa (‘) na nuktakatishi (…) katika uandishi<br>**Imla:** Wasomee wanafunzi habari kwa vituo ili waandike kwa | Kifungu cha habari kimeandikwa kwa usahihi kwa kuzingatia alama za uakifishaji nuktapacha (:), nuktamkato (;), ritifaa (‘) na nuktakatishi (…) | Barua za kiofisi, kompyuta, kamusi na kadi za alama za uakifishaji | 22 |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 44 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | kuzingatia alama za uakifishaji: nuktapacha (:), nuktamkato (;), ritifaa (‘) na nuktakatishi (…) | | | |
| | | (b) Kutumia msamiati sahihi katika uandishi wa insha kwa kuzingatia mada | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kujadili na kuandika wazo la kila aya, kisha wakamilishe insha kwa kutumia msamiati mwafaka | Msamiati sahihi umetumiwa vizuri katika uandishi wa insha kwa kuzingatia mada | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kuandika barua ya kiofisi kwa kuzingatia muundo sahihi | **Majigambo:** Wape wanafunzi uhusika kwa vikundi kulingana na vipengele vya barua ya kiofisi, kisha waongoze kujigamba<br><br>**Maswali na Majibu:** Waongoze wanafunzi kuandika barua za kiofisi kwa kuzingatia vipengele vyake | Barua ya kiofisi imeandikwa kwa usahihi kwa kuzingatia muundo wake | | |
| 2.0 Kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma | 2.1 Kuonesha stadi za kusikiliza na kuelewa | (a) Kusimulia hadithi aliyoisikiliza kwa usahihi | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kujadili mambo ya msingi wakati wa kusimulia hadithi | Hadithi iliyosikilizwa imesimuliwa kwa usahihi | Hadithi, redio, kamusi, tableti, sidii na kompyuta | 22 |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 46 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Masimulizi:** Waongoze wanafunzi kuhadithia maisha yao wakati wa likizo | | | |
| | | (b) Kutafsiri ujumbe mkuu uliomo kwenye hadithi na mazingira halisi | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kueleza mafunzo wanayoyapata kutokana na hadithi kwa kuwauliza maswali<br>**Bakuli la samaki:** Waongoze wanafunzi kukaa katika maduara mawili (duara ndani na duara nje), | Ujumbe mkuu uliomo kwenye hadithi umetafsiriwa kwa usahihi kwa kuzingatia mazingira halisi | | |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 47 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | kisha wale wa ndani waeleze mafunzo wanayopata kwenye hadithi na wale wa nje waongeze kile kinachopungua | | | |
| | | (c) Kuhusianisha mienendo ya wahusika waliomo katika hadithi na mazingira halisi | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili mienendo ya wahusika inavyoshabihiana na mazingira halisi<br>**Uchunguzi:** Wape wanafunzi wasifu wa kila mhusika, kisha waongoze kuchunguza kwa kulinganisha na watu katika jamii yao | Mienendo ya wahusika waliomo katika hadithi imehusianishwa na mazingira halisi kwa usahihi | | |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 48 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) Kufafanua maana ya nahau na methali zilizomo katika hadithi kwa usahihi | **Mchezo:** Andaa kadi mbili kubwa, moja iandikwe neno "nahau" na nyingine iandikwe neno "methali", kisha andika nahau na methali nyingi katika karatasi tofautitofauti, halafu waongoze wanafunzi wenye kadi zilizoandikwa nahau kusimama mbele ya kadi kubwa iliyoandikwa 'nahau' huku wakizinyanyua, na wale wenye kadi zilizoandikwa methali wafanye hivyohivyo | Maana ya nahau na methali zilizomo katika hadithi zimefafanuliwa kwa usahihi | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Mchezo:** Unda timu mbili, kisha timu moja iwe inataja nahau na timu ya pili iseme maana yake. Pia, ifanyike kwa methali kwa kubadilishana utendaji | | | |
| | 2.2 Kusoma matini kwa ufasaha na ufahamu | (a) Kusoma matini ndefu sahili | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kusoma matini ndefu sahili, kisha waulize wanafunzi maswali kuhusu matini hizo<br><br>**Kazimradi:** Waongoze wanafunzi kutembelea maktaba kusoma matini ndefu sahili, kisha wabainishe mawazo yaliyomo katika matini hizo na kuwasilisha darasani | Matini ndefu sahili zimesomwa kwa ufahamu | Matini bunifu na zisizo bunifu ndefu sahili | 22 |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 50 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kuwasilisha mawazo makuu aliyoyasoma katika matini ndefu | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kusoma matini, kisha waeleze mawazo makuu waliyojifunza<br><br>**Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kujadili mawazo makuu katika matini ndefu waliyoisoma | Mawazo yaliyosomwa katika matini ndefu yamewasilishwa kwa usahihi | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3.0 Kuwasilisha hoja kwa mazungumzo na kwa maandishi kulingana na muktadha | 3.1 Kuwasilisha hoja kwa njia ya mazungumzo katika miktadha mbalimbali | (a) Kutoa hoja kwa kutumia msamiati unaoendana na muktadha mahususi wa mazungumzo | **Igizo:** Waongoze wanafunzi kuigiza kuwasilisha hoja katika kikao cha serikali ya wanafunzi<br><br>**Kualika mgeni:** Mwalike Afisa Maendeleo ya Jamii kutoa mada kuhusu afya au mahusiano sahihi ya kijinsia, kisha waongoze wanafunzi kuchangia hoja kutokana na mada iliyowasilishwa | Hoja zimetolewa kwa kutumia msamiati unaoendana na muktadha mahususi wa mazungumzo kwa usahihi | Vitu halisi, tableti, kompyuta, sidii, picha na redio | 22 |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 52 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 3.2 Kuandika matini mbalimbali | (a) Kuandika insha fupi kwa kuzingatia vipengele vya insha | **Ramani ya dhana:** Waongoze wanafunzi kutaja na kufafanua vipengele vya insha kwa kuanza na mduara wa kwanza wenye neno insha, kisha wao waendelee<br><br>**Oneshombinu:** Onesha insha ya mfano, kisha waongoze wanafunzi kutunga insha kwa kuzingatia mfano huo | Insha fupi imeandikwa kwa kuzingatia vipengele vya insha | Insha mbalimbali, barua za kiofisi, kompyuta, tableti, bahasha na stempu | 22 |

| **Umahiri mkuu** | **Umahiri mahususi** | **Shughuli za ujifunzaji** | **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | **Vigezo vya upimaji** | **Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa** | **Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kujibu barua ya kirafiki | **Maswali na Majibu**: Waongoze wanafunzi kujibu barua ya kirafiki | Barua ya kirafiki imejibiwa kwa usahihi | | |
| | 3.3 Kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali | (a) Kuchambua mawazo mbalimbali yaliyojitokeza katika matini fupi sahili aliyoisoma | **Kazimradi:** Waongoze wanafunzi kutembelea maktaba kusoma matini, kisha wachambue mawazo yaliyomo katika matini walizozisoma | Mawazo mbalimbali yaliyojitokeza katika matini fupi sahili iliyosomwa yamechambuliwa kwa ufasaha | Matini fupi sahili | 22 |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 54 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kueleza mawazo yaliyojitokeza katika matini fupi sahili kwa kuzungumza | **Kusoma matini:** Andaa matini, zigawe kwenye vikundi, kisha waongoze wanafunzi kusoma, kujadili na kueleza mawazo yanayojitokeza katika matini hizo | Mawazo yaliyojitokeza katika matini fupi sahili yameelezwa kwa usahihi kwa kuzungumza | | |
| | | (c) Kufupisha habari alizozisoma katika matini fupi sahili kwa kuandika | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kwa kutumia maswali kubaini mawazo makuu katika matini fupi sahili walizozisoma na kuzifupisha | Habari zilizosomwa katika matini fupi sahili zimefupishwa kwa usahihi kwa kuandika | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 3.4 Kuonesha stadi za awali za ubunifu wa kazi mbalimbali za Kiswahili | (a) Kutunga maigizo rahisi na mafupi kwa kuzingatia kanuni | **Uchunguzi:** Waongoze wanafunzi kuangalia igizo kwenye televisheni au redio na kuchunguza namna wahusika wanavyovaa uhusika katika uigizaji, kisha watunge maigizo rahisi kwa kufuata kanuni<br><br>**Mchezo:** Waongoze wanafunzi kuigiza igizo walilolitunga | Maigizo rahisi na mafupi yametungwa kwa kuzingatia kanuni kwa usahihi | Vitu halisi | 22 |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 56 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kuigiza michezo sahili | **Uchunguzi:** Waongoze wanafunzi kuangalia michezo kwenye televisheni au kusikiliza redioni, kisha wachunguze mbinu za kifani na kuziwasilisha darasani<br><br>**Mchezo:** Waongoze wanafunzi kuigiza maigizo rahisi | Michezo sahili imeigizwa kwa ufanisi | | |

## Darasa la VI

**Jedwali Na. 5**: *Maudhui ya Darasa la VI*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali | 1.1 Kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali | (a) Kutumia msamiati katika mijadala mbalimbali kwa kujiamini | **Mdahalo:** Waongoze wanafunzi kutumia msamiati sahihi katika mdahalo | Msamiati umetumika katika mijadala mbalimbali kwa kujiamini | Televisheni, sidii na redio | 30 |
| | 1.2 Kutumia maandishi katika mawasiliano kulingana na miktadha mbalimbali | (a) Kubaini makosa ya kiuandishi katika matini | **Uchunguzi:** Waongoze wanafunzi kusoma matini kwa umakini na kubainisha makosa ya kiuandishi | Makosa ya kiuandishi katika matini yamebainishwa | Risala, hotuba, kompyuta, tableti na matini mbalimbali | 30 |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 58 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kusahihisha makosa ya kiuandishi katika matini | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kujadili na kusahihisha makosa kwa kuandika kilichosahihi mahali penye kosa la kiuandishi | Makosa ya kiuandishi katika matini yamesahihishwa | | |
| | | (c) Kuandika risala na hotuba kwa kuzingatia muundo na muktadha | **Kusoma matini:** Waongoze wanafunzi kusoma risala na hotuba mbalimbali, kisha wajadili muundo wa hotuba na risala | Risala na hotuba zimeandikwa kwa kuzingatia muundo na muktadha kwa usahihi | | |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 59 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Majigambo:** Waongoze wanafunzi katika timu mbili kujigamba kuhusu risala na hotuba wakibainisha sifa, muundo, matumizi na wahusika wake. Timu moja iitwe risala na timu ya pili iitwe hotuba<br><br>**Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kujadiliana katika vikundi, mambo ya kuzingatia katika uandishi wa risala na hotuba, kisha waandike risala na hotuba | | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2.0 Kuonesha uelewa wa jambo alilolisikiliza au kulisoma | 2.1 Kuonesha stadi za kusikiliza na kuelewa | (a) Kusikiliza habari mbalimbali na kunukuu mawazo makuu | **Masimulizi:** Waongoze wanafunzi kusikiliza habari ulizoziandaa, kisha waandike mawazo makuu yaliyomo kwenye habari hizo **Uchunguzi:** Waongoze wanafunzi kusikiliza taarifa ya habari kwenye redio/televisheni/ kompyuta, kisha waandike mawazo makuu waliyoyapata | Habari mbalimbali zimesikilizwa na mawazo makuu yamenukuliwa kwa usahihi | Kinasasauti, redio na televisheni | 25 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kufupisha habari alizozisikiliza kwa kuzingatia mawazo makuu | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kubainisha na kuandika wazo kuu kwa kila aya katika habari waliyoisikiliza, kisha waunganishe mawazo na kupata ufupisho | Habari zilizosikilizwa zimefupishwa kwa kuzingatia mawazo makuu | | |
| 3.0 Kuwasilisha hoja kwa mazungumzo na kwa maandishi kulingana na muktadha | 3.1 Kuwasilisha hoja kwa njia ya mazungumzo katika miktadha mbalimbali | (a) Kutumia msamiati mwafaka katika kupinga au kutetea hoja kwa kutoa mifano thabiti kulingana na muktadha | **Mdahalo:** Waongoze wanafunzi kwa kuwapa kichwa cha mdahalo, upande mmoja upinge na mwingine utetee hoja kwa mifano thabiti kulingana na muktadha | Msamiati mwafaka umetumika kwa ufasaha katika kupinga au kutetea hoja kwa kutoa mifano thabiti kulingana na muktadha | Kamusi, televisheni, sidii, redio na kinasasauti | 30 |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 62 12/07/2023 20:42

| **Umahiri mkuu** | **Umahiri mahususi** | **Shughuli za ujifunzaji** | **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | **Vigezo vya upimaji** | **Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa** | **Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kutumia lugha ya mvuto katika kuwasilisha hoja | **Uwasilishaji:** Waongoze wanafunzi kuwasilisha hoja kwa kutumia lugha ya mvuto, yaani yenye tamathali za semi, nahau, methali na misemo | Lugha ya mvuto imetumika kwa usahihi katika kuwasilisha hoja | | |
| | | (c) Kuhutubia kwa lugha fasaha katika miktadha ya shuleni | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kujadili mambo ya msingi ya kuzingatia wakati wa kuhutubia | Kuhutubia kwa lugha fasaha katika muktadha wa shuleni kumefanyika | | |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 63 12/07/2023 20:42

| **Umahiri mkuu** | **Umahiri mahususi** | **Shughuli za ujifunzaji** | **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa** | **Vigezo vya upimaji** | **Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa** | **Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Igizo:** Waongoze wanafunzi kuigiza namna ya kuhutubia kuonesha vipaumbele vyao wakati wa kampeni za kugombea nafasi za uongozi shuleni | | | |
| | 3.2 Kuchanganua mawazo yaliyowasilishwa katika matini mbalimbali | (a) Kusoma mashairi na ngonjera mbalimbali | **Kusoma matini:** Waongoze wanafunzi kusoma matini zenye mashairi na ngonjera | Mashairi na ngonjera mbalimbali zimesomwa kwa ufasaha | Mashairi na ngonjera | 30 |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 64 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Uchunguzi:** Waongoze wanafunzi kusikiliza mashairi na ngonjera zilizorekodiwa, kisha wachunguze namna zinavyotambwa na kughaniwa<br><br>**Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kubainisha mambo ya kuzingatia wakati wa kughani shairi na kutamba ngonjera | | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kuchambua mawazo yanayo jitokeza katika ngonjera na mashairi aliyoyasoma | **Kazimradi:** Waongoze wanafunzi kutembelea maktaba kusoma ngonjera na mashairi, kisha kuchambua ujumbe uliomo<br><br>**Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kufafanua mawazo yaliyojitokeza katika ngonjera na mashairi | Mawazo yanayojitokeza katika ngonjera na mashairi yaliyosomwa yamechambuliwa kwa usahihi | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kusimulia mawazo yaliyomo katika ngonjera na mashairi aliyoyasoma | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kutamba ngonjera na kughani mashairi, kisha wajadili ujumbe uliomo<br><br>**Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi kufafanua mawazo yaliyojitokeza katika ngonjera na mashairi kwa kuwauliza maswali | Mawazo yaliyomo katika ngonjera na mashairi yaliyosomwa yamesimuliwa kwa ufasaha | | |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 67 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 3.3 Kuonesha stadi za awali za ubunifu wa kazi mbalimbali za Kiswahili | (a) Kutunga shairi na ngonjera | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kujadiliana na kuandika maneno yenye miishio inayofanana, kisha waandike maneno yenye mizani nne, halafu waongeze maneno mengine yenye mizani nne (jumla ziwe mizani nane), kisha watunge ngonjera na mashairi kwa kutumia maneno hayo | Ngonjera na mashairi vimetungwa kwa usahihi | Ngonjera, mashairi na vitu halisi | 30 |



MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 68 12/07/2023 20:42

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana/Vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kutamba ngonjera na kughani mashairi | **Uchunguzi:** Waongoze wanafunzi kuangalia ngonjera na mashairi kwenye televisheni na redio na kuchunguza mbinu za kifani zilizotumika<br><br>**Mchezo:** Waongoze wanafunzi kutamba ngonjera na kughani mashairi | Ngonjera zimetambwa na mashairi yameghaniwa kwa usahihi | | |

## Bibliografia


BAKITA. (2013). *Mwongozo kwa waandishi wa Kiswahili sanifu*. BAKITA.

Habwe, J. & Karanja, P. (2004). *Misingi ya sarufi ya Kiswahili*. Phoenix Publishers Ltd.

King'ei, K. (2014). *Taaluma ya uandishi*. The Jomo Kenyatta Foundation.

Massamba, D.P.B., Kihore, Y. M na Hokororo, J. I. (2001). *Sarufi miundo ya Lugha ya Kiswahili sanifu: Sekondari na vyuo. (SAMIKISA)*. TUKI.

Mauritius Institute of Education. (2015). *National curriculum framework grades 1 to 6*.

Mauritius Institute of Education. (2015). *National curriculum framework nine - year continuos basic education.*

Mgullu, R. (2001). *Mtalaa wa isimu: Fonetiki, fonolojia na mofolojia ya Kiswahili*. Longhorn Publishers Ltd.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya uhakiki*. EAEP.

Nkwera, F. (1978). *Sarufi na fasihi, sekondari na vyuo*. Tanzania Publishing House.

Senkoro, F. (1987). *Fasihi na jamii*. Press and Publicity Centre.




MUHTASARI SOMO KISWAHILI DRS III - VI landscape.indd 70 12/07/2023 20:42